

MSHIKAMANO NA USHIRIKIANO WA TUME NA WADAU
WAKE NI MSINGI WA KUBORESHA UTUMISHI
WA UMMA NCHINI.

Imetolewa na ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.

Naibu Katibu Mkuu, Bw. Eric Shitindi (UTUMISHI), kwa niaba ya Katibu Mkuu, Bw. George Yambesi (UTUMISHI) ametoa wito kwa Makamishna, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma kuwa na mahusiano ya karibu na Taasisi za Umma katika utendaji wa kazi zao.

Bw. Shitindi ametoa wito huo wakati alipokuwa akifungua mafunzo ya Makamishna tarehe 13/10/2008 yaliyofanyika katika ukumbi wa Morogoro Hotel. Mafunzo hayo ambayo yanatarajiwa kumalizika leo yalikuwa na lengo la kutoa fursa kwa Makamishna kujifunza kuhusu Sera, Sheria na Kanuni zinazotawala uendeshaji wa masuala ya Ajira na Nidhamu katika Utumishi wa Umma.

Bw. Shitindi ambaye pia alikuwa mgeni Rasmi katika mafunzo hayo amebainisha kuwa mahusiano ya Tume na vyombo vingine vya Serikali yatawawezesha Makamishna kufanya kazi vizuri zaidi na kulinda viwango vya Watumishi, Uwajibikaji na kujenga mazingira ya kuwatumikia wananchi. Aidha, kwa upande mwingine, wadau wa Tume wametakiwa pia kutoa ushirikiano na mshikamano mkubwa na Tume katika utekelezaji wa majukumu yake katika Utumishi wa Umma.

Sanjari na mahusiano hayo Bw. Shitindi amewaomba pia Makamishna katika kutimiza majukumu yao kuzisaidia Mamlaka mbali mbali kuziarifu dosari ili Mamlaka hizo ziweze kuzirekebisha dosari hizo kwa lengo la kuboresha Utumishi wa Umma na kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla.

Akizungumzia kuhusu jitihada za Serikali katika kuboresha Utumishi wa Umma ambazo zilianza mwaka 2000 kwa Programu ya kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma katika Utumishi wa Umma (PSRP), Bw. Shitindi amesema kuwa Tume ya Utumishi wa Umma ni Taasisi muhimu katika maboresho haya na inapaswa kuhakikisha kuwa malengo ya programmu hiyo yanafikiwa kama ilivyopangwa.

Tume ya Utumishi wa Umma huongozwa na Makamishna saba (7) akiwemo Mwenyekiti ambao huteuliwa na Rais. Aidha, Tume ina Katibu, Bibi Thecla W. Shangali ambaye huteuliwa na Rais. Katibu ndio Mtendaji Mkuu na Afisa Mhasibu.

Kama una maoni au maswali,
Tafadhali tuandikie:

**KATIBU,
OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA UMMA,
S.L.P.9143,
DAR ES SALAAM.**